

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA IGUNGA**

**SHULE YA SEKONDARI NANGA,
S.L.P 108,
IGUNGA .
08/12/2020**

MWANAFUNZI
SHULE YA MSINGI

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANGA KIDATO
CHA KWANZA MWAKA 2021.**

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Nanga, Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora.

Unatakiwa kufika Shuleni tarehe 11/01/2020 saa 1:30 asubuhi unapokuja unaombwa uje na mzazi au mlezi wako.

1. SARE

1.1 SARE YA SHULE

a) WASICHANA

- i. Sketi 2 nyeusi zenyе marinda (16) ya kupanga, ziwe zinazofunika miguu usawa wa kifundo cha miguu zisizobana mwili, mkanda usiozidi inch (2) kitambaa kizito
- ii. Shati mbili rangi nyeupe za mikono mifupi zisibane mwili.
- iii. Shati/blauzi ichomekewe ndani ya sketi wakati wote
- iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vyenye kutumia kiwi na sio petrol vyenye visigino vifupi viatu vya ghorofa HAVIRUHUSIWI
- v. Soksi nyeupe jozi mbili(NDEFU)
- vi. Tai 1 nyeusi (ndefu)
- vi. Sweta 1 damu ya Mzee
- vii. Wanafunzi wa kiislamu: sketi (2) ziwe ndefu usawa wa kifundo cha miguu zenyе marinda (16) ya kupanga na nusu kanzu iwe ndefu pia.

b) WAVULANA

- i. Suruali mbili (2) nyeusi kulingana na urefu wako na pana ya kutosha hatuhitaji ya kubana na mifuko ni ya pemberi, siyo ya mbele aina ya (pisto)iwe na marida. Uvaaji wa suruali chini ya makalio MTEPESHO ni MARUFUKU
- ii. Mashati mawili(2) meupe ya mikono mifupi
- iii. Mkanda mweusi wa ngozi usiwe na picha/urembo wowote
- iv. Tai 1 nyeusi ndefu
- v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vyenye kutumia kiwi na sio petrol, viwe na visigino vifupi, viatu vya ghorofa HAVIRUHUSIWI
- vi. Sweta 1 rangi ya damu ya mzee

vii. Soksi nyeupe jozi mbili

1.2 **NGUO/SARE ZA MICHEZO NA KAZI**

a) **WASICHANA**

- i. T. shirt (fulana) 2 moja nyekundu na njano moja zenyenembo ya shule.
- ii. Sketi mbili (1) light blue na nyingine nyekundu (1). Ashone kwa kufuata maelekezo kama yale ya sketi nyeusi (kitambaa kizito)
- iii. Raba za kuvaan wakati wa michezo kazi na wakati wa masomo ya jioni rangi yoyote

b) **WAVULANA**

- i. T.shirt 2 moja nyekundu na moja njano zenyenembo ya shule.
- ii. Suruali mbili za rangi ya zambarau zishonwe kama suruali nyeusi. Hatua kali zitachukuliwa kwa ambaye hatazingatia masharti ya ushonaji
- iii. Raba za kuvaan wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo jioni rangi yoyote

VIFAA KWA AJILI YA MASOMO.

- i) Madaftari yasiyopungua 15 makubwa.(**counter books**)
- ii) Mathematical set 1
- iii) Kalamu, penseli na mfutio.
- iv) Madaftari madogo kwa ajili ya mazoezi na majoribio
- v) Jalada la kuhifadhia mitihani yake (file)
- vi) Dictionary 1 (English)

1.3 **UCHANGIAJI WA CHAKULA**

Utaratibu uliokubaliwa na wazazi wa wanafunzi kupatiwa chakula cha mchana unawahusu wanafunzi wote. Kwa hiyo, kwa muhula wa kwanza unatakiwa kuchangia mahitaji yafuatayo:

- (i) Mahindi debe $1 \frac{1}{4}$
- (ii) Maharage kilo $6 \frac{1}{2}$
- (iii) Mafuta ya kupikia lita $1 \frac{1}{4}$
- (iv) Chumvi $\frac{1}{4}$ ya kilo
- (v) Sukari kilo $1 \frac{1}{4}$
- (vi)** Fedha taslimu 3,600/=

Mchango hupokelewa na wajumbe wa kamati ya chakula siku za jumatatu, jumatano na ijuma isipokuwa siku ya sikukuu.

1.4 **USALAMA NA USTAWI WA MWANAFUNZI**

Kwa kuwa wanafunzi wote husoma wakitokea nyumbani, ni wajibu wa wazazi kuhakikisha usalama na ustawi wa mwanafunzi kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Kuhakikisha mwanafunzi anakuwa na mahali salama pa kuishi kwa wanafunzi wanaolazimika kupangishiwa mahali pa kukaa. Mzazi atakuja na maelezo ya wapi anakoishi mtoto, namba za simu za mmiliki wa nyumba na kiongozi wa kitongoji.
- (ii) Wazazi wanaoishi na Watoto wao nyumbani wanawajibika kuweka utaratibu wa usafiri. Ni MARUFUKU wanafunzi kubebwa na malori ya mizigo au magari ya watu binafsi

wasiofanya biashara ya usafirishaji. Wanafunzi wenye uwezo wa kuendesha baiskeli wanashauriwa wapatiwe usafiri huo.

2. MAKOSA YAFUATAYO YAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

Mwanafunzi atakaye patikana na kosa mojawapo kati ya haya yafuatayo atakuwa amejifukuzisha Shule

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
- iii. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevyta
- iv. Uvutaji wa bangi
- v. Makosa ya jinai
- vi. Kupiga au kupigana
- vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- viii. Kudharau Bendera ya Taifa
- ix. Kuoa au kuolewa
- x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- xi. Kutoa mimba
- xii. Kugoma, kuchocheara na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
- xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiv. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na uylatekeleze kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



**STEPHEN J. MZIMYA
MKUU WA SHULE**

NB: kabla ya kumleta mwanafunzi shulenii hakikisha umempeleka hospitali kwa ajili ya kuchunguzwa afya na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa.

THE MEDICAL EXAMINATION FORM SHOULD BE COMPLETED BY GOVERNMENT
MEDICAL OFFICER

FROM THE HEADMASTER

NANGA SECONDARY SCHOOL

P.O BOX 108,

IGUNGA

Mobile 0755428626 / 0627015250

TO THE MEDICAL OFFICER

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government medical officer)

Please examine the above named person as to his/her physical and mental fitness for full time learning.

- a) Eye
Sight.....
- b) Hearing.....
- c) Limb.....
- d) Speech.....
- e) Venereal
Diseases.....
- f) Leprosy.....
- g) Epilepsy
.....
- h) Blood
Test.....
- i) Stool
Examination.....
- j) T.S
Test.....
- k) Asthma.....
- l) Anaemia.....
- m) Chest.....
...
- n) Operations
.....
- o) Serious Accidents
.....
- p) Any Other Infection
Neuroses.....
.....
Other Serious Diseases
.....
Pregnancy
.....

The diagnosis reveals that the above named person is physically and mentally fit/ unfit for full time studying

Name and signatures of the medical Officer.

_____ date _____